

**JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILALA YA MURANG'A KUSINI 2016****INSHA****102/1****MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

1. (a) Hii ni insha ya dayalojia.  
Sura ya dayalojia izingatiwe yaani ya kitamthilia.
- (b) Dayalojia izingatie sehemu zifuatazo;  
(i) Kichwa / Anwani.  
Kichwa kiandikwe kikamilifu kwa kutaja kuwa ni dayalojia.  
Wanaoshiriki katika dayalojia watajwe. Kichwa pia kionyeshe mada inayozungumiziwa.
- (ii) Utangulizi.  
Haya ni maelezo mafupi kuhusu mandhari.
- (iii) Suala.  
Suala ni kuhusu usalama yaani jinsi ya kuimarisha usalama.
- (iv) Wahusika.  
Wahusika wafuatwe na koloni.
- (v) Maelezo mafupi.

Haya huwa kwa mabano ili kueleza hali ya wanaoshiriki.

Hoja

- Jamii ielimishwe kuhusu umuhimu wa kudumisha usalama na kuwashika wahalifu.
- Kuongeza idadi ya askari / walinda usalama. Kuwapa polisi vifaa vya kazi vya kutosha.
- Kuwajibika kwa askari kazini.
- Kuimarisha uchumi / mikakati ya kuongezea nafasi za kazi.
- Kuimarisha korti zetu mahakama, jela na kadhalika.

Tanbihi

Hoja ni lazima zijenge maudhui aliyopewa.  
Hoja zijengwe kwenye misingi ya ukweli.  
Mtahiniwa asipozingatia sura ondoa alama 4 za sura

2. (i) Hii ni insha ya mjadala.
- (ii) Mtahiniwa anafaa kuzungumzia kuhusu faida na hasara za simu tampa.  
Inafaa ajadili pande mbili.
- (iii) Mtahiniwa awe na angalau hoja tano ambazo zimefanuliwa.

Hoja za faida

- Imerahisisha kazi ya wanabiashara.
- Katika dharura kuna nambari maalum za kuomba usaizidi.
- Husaidia watu kupanga siku zao vizuri.
- Hukumbusha watu kuhusu matukio muhimu yanayotazamiwa.
- Unaweza kujua pesa zinazohitajika kwa huduma kama nguvu za umeme kwa ujumbe wa rununu.

Hasara

- Madereva wanaoshika usukani huku wanawasiliana husababisha ajali.
- Baadhi ya watumizi wake huzungumza bila adabu hadharani bila kujali walipo (hospitalini, kwenye benki na kadhalika)
- Wengine hutoa siri zao hadharani na kuhatarisha maisha yao.
- Zimesababisha sintofahamu katika ndoa na familia.
- Hatari za kiafya zinaweza kutokeea.
- Udanganyifu kwenye mitihani.

3. (i) Hii ni insha ya methali. Hisani haozi.
  - (ii) Kisa kidhihirishe maana ya methali.
  - (iii) Maana ni kuwa ukitenda wema, wema huo haupotei hivi hivi tu.  
Huenda na wewe ukalipwa wema huohuo ulioutenda.
- Kisa kinaweza kuzungumizia mhusika ambaye alitenda wema wakati fulani. Mhusika huyo naye baadaye akatendewa wema ambaa ulimfaa katika maisha yake.

(a) Kisa kiwe na pande mbili:

- (i) Upande mmoja uwe ni kuhusu wema ambaa mhusika aliufanya au kuutenda.
- (ii) Upande wa pili uwe kuhusu wema ambaa mhusika yuyo huyo alitendewa.

- (b) Mtahiniwa akiegemea upande mmoja atakuwa amepungukiwa kimaudhui japo hajapotoka

(c) Mtahiniwa ambaye ataandika kisa kisichooana kabisa na methali atakuwa amepotoka kumaudhui.

4. (i) Hii ni insha ya mdokezo.
- (ii) Maneno kiini katika swalii hili ni kuaibika kuhusu kitendo fulani.  
Hali inayodhilihirika ni ya aibu.
- (iii) Kisa kidhihirishe kitendo ambacho kinamfanya mhusika kuaibika.
- (iv) Mtahiniwa anaweza kurudi nyuma kwa kutumia mbinu rejeshi na kusimulia hadi anapofikia hali hii yakuaibika.
- (v) Nafsi ambayo itatawala katika insha hii ni nafsi ya kwanza.

**JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILALA YA MURANG'A KUSINI 2016****102/2****LUGHA****MWONGOZO WA KUSAHIHISHA****Ufahamu.**

1. Anwani.  
Mbinu za kujifunza kwa makundi. *al 2*
2. Huwafanya wanafunzi wanaoonekana kuwa na uwezo wa chini kujumuika na wale wanaoonekana kuwa na uwezo wa juu. *al 2*
3. (i) Idadi yao  
(ii) Uwezo wao  
(iii) Mtazamo wa mwalimu wao. *al 3*
4. Manufaa.  
- Kuchangizana maarifa.  
- Kupata maarifa wasiyokuwa nayo.  
- Kutambua mambo mapya au makosa vitabuni.  
- Kukuza ujasiri.  
- Umoja na utangamano. *al 4*
5. (i) Wanafunzi kupata himizo kutoka kwa wenzao.  
(ii) Mwalimu kuwaeleza wanafunzi kuwasilisha hoja zao mbele ya wenzao *al 2*
6. (i) Marafiki wa karibu.  
(ii) Shughuli ya marudio. *al 2*

**2. Ufupisho.**

- (a)
- Ufunzaji wa muziki nyumbani na shuleni una manufaa mengi.
  - Muziki ni kutulizo kikubwa sawa cha moyo wabinadamu.
  - Muziki una njia ya kipekee ya kuwasiliana.
  - Muziki humsaidia mtoto kuendeleza hisia nzuri zakuburudisha na za kuzuzua.
  - Humwezesha kukabiliana na tajriba mbaya.
  - Humpa fursa ya kutoa moyoni simanzi na dhiki yakena hivyo kumrejeshea raha tena. *al 6 ut 2*
- (b)
- Watoto hujipatia mbinu za werevu shuleni haswa kwenye somo la hesabu na mambo mengine kwa ujumla.
  - Watu wazima waliojifunza muziki kabla ya umri wamiaka 12 huwa na utumizi mzuri wa maneno magumu na msamati kuliko wale ambao hawakujifuuza kuimba.
  - Pia husaidia watoto walio na kasoro za kuzungumza au wenye ulimi mzito wa kuzungumza kujieleza kwa ufasaha kupitia kwa muziki.
  - Wenye shida ya kigugumizi huweza kujiamini, kujifunza na kuelewa mila na tamaduni zao. *al 6, ut 1*

**3. Lugha.**

1. Sauti /th/  
Ni kikwamizo hafifu / sighuna cha meno.
2. Viambishi tamati.  
ew - kiambishi tamati cha kauli (kutendewa)  
a - kiambishi tamati kiishio. *al 2*
3.  
- Kiambishi kikanushi - Ha  
- Kiambishi cha hali timilifu - ja  
- Kiambishi ch amtendewa - m  
- Mzizi wa kitenzi - pig  
- Kauli ya kutendea - i  
- Kitamatishi - a *al 4*
4. Aina za shamirisho.  
Shimirisho kipozi : gilasi ya maji  
Shimirisho kitondo : kiambishi "wa" wao *al 2*
5. Kasisi alipoingia kanisani : kishazi tegemezi  
Waumini walianza kushangilia : kishazi huru *al 2*
6. Matumizi ya "ni"

- (i) Wahusika wengi wanaoamrishwa. Rudini  
 (ii) Kielezi cha mahali - uwanjani  
 (iii) Yambwa / shamirisho (Nafsi ya kwanza)  
 Mimi - mkanifutie.

(iv) Kitensi kishirikishi - ni *al 2*

7. Aina za vivumishi.

- (i) Chochote : kiyumishi cha pekee  
 (ii) ii hii : kiyumishi kisisitizi *al 2*

8. Kiambi "ji"

Mifano.

Jilinde

Jinunulie

*al 2*

9. Kuchanganua kwa jedwali.

Sentensi Ambatano

S <sub>1</sub>			U	S <sub>2</sub>	
KN	KT			KN	KT
Φ	T	E		Φ	T
Φ	Alienda	usiku	ingawa	Φ	nilimtahadharisha

10. Mzazi alimuuliza mhisani kama wangeweza kumsaidia mtoto wake siku ambayo ingefuata. *al 3*

11. (i) -la (kutendeshea) - lishia

*al 2*

(ii) Toa (Tendeka) – Toleka

12. (i) Alama ya hisi (!)

Hutumika kuonyesha hisia mbalimbali kama vile mshangao, huzuni, furaha, kushtuka na kadhalika

(ii) Parandesi / mabano [ ] ( )

(a) Kuonyesha maneno yasiyokuwa ya lazima.

Mfano

Wanariadha wa Kenya (na ni wengi kweli kweli) wametuzwa zawadi.

(b) Kuzingira nambari na herufi (i)

13. Ukubwa (wingi)

Magoma haya yatachezwa nyanjani. *al 2*

14. Vijakazi wawa hawa walizipoteza funguo zizi hizi licha ya kukanya. *al 2*

15. Haliya - a-

Chui ala swara *al 2*

16. Aina za virai.

(i) wa kijinsia : kirai kiyumishi

(ii) viongozi wenye msimamo thabiti mno;

kirai nomino *al 2*

17. 'O' rejeshi tamati

Kiatu kinunuliwacho si kile ukitakacho *al 1*

18. Kuyakinisha (nafsi ya tatu umoja)

Akionana na mzazi atapata pesa *al 2*

#### 4. Isimujamii. (al 10)

(i) Sajili ya magazeti / uanahabari. *al 2*

(ii) Sifa za sajili ya magazeti.

(a) Huwa na anwani fupi zenyen mvuto.

(b) Hutumia lugha sanifu.

(c) Huwa na aya fupi zenyen kubeba ujumbe kikamilifu.

(d) Huweza kutumia picha.

(e) Lugha ni rahisi kuelewaka.

(f) Masuala mengine huwa ni ya kitaaluma.

(g) Usemi halisi huweza kutumiwa kuwanukuu wasemaji.

(h) Vijichwa hutumiwa

(i) Habari zingine huwa ni za uongo ili kuwaharibia sifa walengwa.

(g) Chuku hutumika katika baadhi ya makala ikinuia kuyapa makala uzito zaidi.

(k) Makala huchukua mtindo wa ripoti. *al 8*

**JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILALA YA MURANG'A KUSINI 2016****102/3****KARATASI YA TATU****MWONGOZO WA KUSAHIHISHA****Ushairi.****1. Lazima.**

(a) Kichwa cha ushairi.

Malenga / watanzi wa kike mu wapi? *al 2***(b) Bahari.**

(i) Ukara

(ii) Tarbia / unne

(iii) Mathnawi

*al 2*(c) (i) Idadi sawa ya mishoro katika kila ubeti / minne  
katika kila ubeti.

(ii) Kuna urari wa vina.

Ndani ni - si

Nje ni - ri

(iii) Kila ubeti una kibwagizo.

(iii) Idadi sawa ya mizani kwa kila mshororo / mizani  
kwa kila mshororo / mizani 16 kwa kila mshororo(v) Lina ukwapi na utao / vipande viwili kwa kila mshororo. *al 4***(d) Maudhui**

Watu wa jinsia ya kike / wanawake wamekataakushiriki katika utunzi wa mashairi licha ya kuwa wanavyo vipawa / talanta

*al 2***(e) Toni**

Toni ya kulalamika : Haya yaso ufanisi.

Toni ya ukali au hasira : Umalenga u kuasi. *al 2***(f) Lugha ya nathari.**Naichukua nafasi hii ili kukariri na kufichua upesi mambo ambayo kamwe si siri. Msikilize niwapashe habari hii kuhusu  
ugani wa mashairi mko wapi watanzi wa kike? *al 4***(g) Idhini ya kishairi.**

(i) Inkisari.

Ndaningu - badala ya ndani yangu

i - badala ya hii

(ii) lahaja - hino badala ya hii

(iii) utohozi - peni badala ya kalamu

*al 2***(h) (i) Mwatughasi - mwtuuudhi**

(ii) Utensi - malalamiko

*al 2***2. Riwava****(a) Kueleza muktadha.**

Msemaji ni askari immoja wa Mtemi.

Msemezwa ni askari mwagine wa Mtemi.

Mandhari ni nje ya ofisi ya Mtemi Nasaba Bora.

Amani na Imani walikuwa wameshikwa kwa

tuhuma za kuua kitoto Uhuru. Walipigwa

kumbo na kuelekezwa kwenye seli.

*al 4***(b) Mbinu na tamathali za lugha.**

(i) Methali : leo ni leo asemaye kesho ni mwongo.

(ii) Msemo : kuona cha mtema kuni. *al 2***(c) Uozo**

- Imani na Amani waliteseka mno kutokana nauovu wa Mtemi wa Nasaba Bora.

- Mtemi Nasaba Bora akiwa waziri wa ardhalibadilisha hati za wamiliki halali na kuunda zake

- Udhaliimu ulimfanya mamake Imani apigwe na askari katili, kipigo kinasababisha kifo.

- Kuharibu mali ya umma. Kuchoma nyumba ya akina Imani.

- Katika wizara ya ardhi na makao Nasaba Bora anakula mlungula.

- Ufisadi kupitia Nasaba Bora kumtaututia mwanawе Madhubuti kazi katika jeshi.

- Kuwatoza raia pesa ili mtoto wa Nasaba Borakusomea Urusi.

- Uzembe. Baadhi ya wafanyakazi ni wazembe kwa mfano wale wauguzi.

- Uasherati. Nasaba Bora kuwa na uhusiano wa kimpenzi nje ya ndoa.

- Undanganyifu. Fao kufanyiwa mitihani yake.

- Oscar Kambona kuwa mhalifu na kuwa mraibu wa mihadarati, baada ya kunyang'anywa shamba lao.
- Wizi wa mali ya umma. Mtemi Nasaba Bora kunyakua mali ya Chichiri Hamadi na Mwinyihatibusi Mtembezi.
- Nasaba Bora kumnyanyasa Amani kwa kumsukumia kitoto kichanga kisichomhusu ndewe wala sikio.

*zozote 7 x 2 = al 14*

3.(a) Sadfa

- Matukio mawili yanayotokea bila kupangwa na yakaleta athari fulani.
- Kukutana kwa Amani na Imani kulikuwa sadfa. Sadfa hiyo ilimzuia Imani kutitosa kwenye ziwa Mawewa.
- Ni sadfa kuwa Amani alikuwa anataka kupata kazi kwa Mtemi Nasaba Bora. Anapofika mchungaji na mkamaji ng'ombe alikuwa mgonjwa, Amani akapata nafasi.
- Imani alipoipata barua kutoka kwa Amani kuhusu mswada alioibiwa, aliiwa na Dora akausahau mezani. Majisifu aliikuta na kuisomana akajua kuwa Imani ndiye mwandishi wa kile kitabu.
- Gaddafi na wenzake walipotaka kumuua Mtemi Nasaba Bora. Amani alitokea na kumshurutisha Gaddafi asimuue.
- Kukutana kwa Amani, Imani na Bob D.J karibuna mto Kiberenge. Bob DJ anawaelekeza Amani na Imani nyumbani mwa Mtemi Nasaba ora.

*5 x 2 = 10*

(b) Jazada

- Anwani ya kitabu na jazanda.  
Inarejelea wahusika fulani kuharibikiwa na mambo fulani.
- Kuzaliwa na kufa kwa mtoto Uhuru.  
Anawakilisha Uhuru kapatikana kufa kwake nijinsi wananchi wananyanyaswa na kudhulumiwa- hakuna uhuru.
- Fahali mweusi kutafuna kaptura.  
Fahali mweusi ni Mtemi Nasaba Bora anavyonyakua mali ya raia.
- Radi na moto kusimamia kisasi alichonua kulipiza Oscar Kambona.
- Kumnyonyoa kipungu manyoya.  
Ni kumshusha hadhi na kumwondo Mte mamlakani.
- Angurumapo simba mcheza nani?  
Mtemi ndiye simba na atoapo amri hakuna anayeweza kupinga.
- Kunusurika kifo kwa Amani, Imani na D.J
- Ni kutofifisha juhudzi za ukombozi.

*5 x 2 = 10*

4. (a) Muktadha.

Msemaji ni Beka.

Msemezwa ni Mstahiki Meya

Mandhari ni ofisini mwa Meya.

Wawakilishi wa wafanyakazi wamepeleka malamishi yao kwa Meya ili ayashughulikie. Hata hivyo Meya hakuyashughulikia. Alisema hakuna pesa. *al 4*

(b) Msemo

Kazi ya kijungujiko *1 x 2 = 2*

(c) Mbinu za wanacheneo za kujikomboa.

- Kuchaguliwa kwa wawakilishi wa wafanyakazi.  
(Tatu, Beka na Medi)
- Migomo. Waliandaa migomo kama njia ya kushughulikia shida zao.
- Daktari Siki kuchukua jukumu mwenyewe la kupeleka malalamishi ya wanacheneo kwa Meya
- Wanahabari walichangia kufahamisha wanacheneo kuwa shida zao zinatokana na uongozi mbaya wa Meya.
- Diwani III na Daktari Siki kuungana ili kupigania maslahi ya wanacheneo.
- Diwani III kupinga mipango mbalimbali ya Meya na kutaka wanacheneo kushughulikiwa.
- Wafanyakazi kuungana katika mgomo hadi kusababisha kung'atuliwa kwa Mstahiki Meya uongozini.

*7 x 2 = 14*

5. (a) Msemaji ni Daktari Siki.

Msemewa ni Mstahiki Meya

MMahali ni nyumbani mwa Meya.

Sababu : Daktari Siki analalamikia matatizo wanayopitia wanacheneo.

*4 x 1 = 4*

(b) Mbinu za kuendeleza utawala wa Meya.

- Propaganda.

Vijana kushiriki katika mashindano ya nyimbo kisha kupewa zawadi ndogondogo na kuonyehswa kwenye runinga.

- Ahadi za ungo.

Dawa ziko kwenye hahari kuu na zingefika baada ya siku tatu.

- Sheria kandamizi.

Riot Act, Mayors Act na Collective responsibility.

- Vibaraka kuzawaadiwa.k.v

Diwani I na Diwani II

- Kutumia vyombo vya dola.

Matumizi ya askari.

- Kupuzilia mbali malalamishi ya wanacheneo.
  - Kutumia unafiki wa kidini.
  - Matumizi ya vitisho.
6. (a) Haya ni maneno ya msimulizi kwa jina.  
 Abu - Hii ni baada ya Abu kuamua kujaribu bahati yake katika harkati za kuasi ukapera.  
 Mwanzoni hakuridhia kwa kuwa hakuwa amesahau vile posa yake ya awali iliviyokataliwa.  
 Jamaa wake walimrai amwoe Amali. Alikubalikumtwaa Amali awe mpenzi wake hata ingawa alighairi baada ya mipango yote kukamilika.  
*(al 4)*

- (b) Tashbihi.  
 Kuwa kama mtu aliyona unyasi baada ya *al 2*  
 kuumwa na nyoka.

- (c) Nafasi ya mwanamke.  
  - Ni waimbaji  
 Wanamwimbia Abu anapowasili katika makaoya harusi.
  - Ni watamaduni  
 Wanahakikisha kuwa taratibu zote za kindoa zinafanyika chini ya utamaduni wao.
  - Ni wabaguzi  
 Zena anambagua Abu kwa msingi wa umaskini.
  - Ni walezi bora  
 Zena amempa Amali malezi bora hadi kufikiwa kuolewa.
  - Ni waandalizi bora  
 Wanahakikisha maandalizi bora katika ndoa ya Abu na Amani.

*5 x 2 = 10*

- (d) Mbinu ya kinaya.  
  - Abi kuambiwa na binamu yake achangamke wanapoelekea nyumbani kwa akina Amali.
  - Abu na wenzake kukaribishwa kwa nyimbo naakina mama.
  - Wazazi wa Amali kumkatalia posa Abu mara ya kwanza na kukubali mara ya pili.
  - Abu kuraiwa na jamaa zake amwoe Amali lichaya posa kukataliwa mara ya kwanza.
  - Abu kumwacha Amali.
  - Ni kinaya Fahami na jamaa wengine kuambiwa na Abu waende nyumbani. *al 4*

7. (a) Maana  
 Maigizo ni sanaa ambayo wahusika wake au watendaji huiga vitendo vya watu mbalimbali katika jamii na aina nyingine za viumbe ili kupasha ujumbe fulani kwa hadhira.  
*al 2*

- (b) Aina mbili kuu za maigizo.  
 (i) Sanaa ya maonyesho.  
 (ii) Maigizo ya kawaida.  
 Sanaa ya kawaida / maigizo ya kawaida;  
  - Huwa na jukwaa malum.
  - Hutendeka wakati maalum.
  - Huwa na lengo maalum.
  - Ni nje ya mazingira, wakati na hali halisi Sanaa ya maonyesho;
  - Huwa na matendo ya ulimwengu halisi.
  - Mazingira halisi huwa bayana.
  - Laweza kutokea au kutendeka mahali popote.
  - Washiriki ndio hadhira.

- (c) Umuhimu wa maigizo.  
  - Hukuza na kuendeleza vipawa vya waigizaji.
  - Ni njia ya kuendeleza maadili katika jamii.
  - Huwapawatu ujuzi na stadi mbalimbali katikamaisha.
  - Ni njia moja wapo ya kuelimisha wanajamii kwamambo mbalimbali.
  - Huburudisha. Ni burudani kwa hadhira.
  - Ni mbinu mojawapo ya kujifunza na kujiendeleza katika matumizi ya lugha husika. *4 x 1 = 4*

- (b) Dhima ya nyiso.  
  - Kujasirisha. Huwapa vijana ujasiri wa kukabiliana na kisu cha ngariba.
  - Wahusika hufunzwa kuhusu majukumu mapya.
  - Hutumika katika kukuza na kuelimisha kuhusu utamaduni.
  - Huleta umoja na utangamano.
  - Ni njia ya kuonyesha kuwa mhusika ametoka utotoni hadi utu uzima.
  - Hubeza na kukejeli wasiopitia sherehe kama hii na wanaoonyesha ishara za uoga.
  - Huburudisha wanaoshiriki na wanaohudhuria. *5 x 2 = 10*